

ONJENI MWONE

Zab 33 ,2-3,4-5,6-7,8-9;Zab 33,2-3,10-11,12-13,14-15;Zab 33,2-3,16-17,20-21,22-23

Usage Liturgique :-Siku ya Mungu ya Kumi na Kenda katika mwaka B :couplets 1-4

Siku ya Mungu ya Makumi Mawili katika mwaka B :couplets 1 ,5-7

Siku ya Mungu ya makumi Mawili na Moja katika mwaka B :couplets 1 , 8-10

Musique : Bisimwa Bienvenu

O nje ni, mwo ne ji nsi Bwa na a li vyo mwe ma

- 1 . Nitamtukuza Bwana kila wakati ;sifa yake kinywani mwangu siku **zote**.
Roho yangu ijisifu katika Bwana : wanyonge wasikie naku **furahi**.
2. Mtukuzeni Bwana pamoja nami ;tulikuze jina lake wote pamoja.
Nalimkimbilia Bwana, akani sikiliza , akaniopowa katika hofu zangu **zote**.
3. Mtazameni yeye mkafurahiwe ,wala nyuso zenu zisihuzu**nike**.
Mnyonge huyu alilia ,naye Bwana akasikia ,akamwoko katika shida zake **zote**.
4. Malaika wa Bwana amepanga jeshi kando zote za wenye kumeha ,akawa**opowa**.
Oneni ,mwonje jinsi Bwana alivyo mwema ; heri mtu yule anaye mkim**ilia**.
5. Mheshimu Bwana enyi watakatifu wake ,kwa maana wenye kumheshimu hawakosi **kitu**.
Watajiri wamegeuka maskini , wakaona njaa ; bali wanaomtafuta Bwana hawakosikitu **chema** .
6. Njoni , waana , mmisikie ; nitawafundisha kumheshimu **Bwana** .
Ni nani mtu anayependa uzima , anayetaka siku zake za kuona **heri**?
7. Zuilia ulimi wako ubaya , na midomo yako isiseme **uwongo**.
Uepuke na mabaya ,utende mema , tafuta amani na kuifu**atia**.
8. Macho yaBwana yawaangalia watenda mema,na masikio yake yaelekea milio **yao**.
Uso wa Bwana ni juu watenda mabaya , ili angoe ukumbusho wao dun**iani**.
9. Mateso ya mtu mwema ni mengi ,lakini Bwana amwopoa katika **yote**.
Ailinda mifupa yake yote : hata mmoja wake hautavun**jika**.
10. Ubaya unamwua mtu mwovu , nao wenye kumchukia mtu mwema watapatil**izwa**.
Bwana anakomboa roho za watumishi wake , wote waliomkimbilia hawatapatil**izwa kamwe**.